# JARIDA LA MWEZI

TOLEO NA. 056

JUNI 2025

TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY




## 1 MKUU WA MAKAPTENI ZANZIBAR AELEZEA MIPANGO YA SAFARI INAVYOTEGEMEA TAARIFA ZA HALI YA HEWA

## 2 DKT. CHANG'A ASHIRIKI MKUTANO WA 62 WA KAMATI YA UTEKELEZAJI WA MKATABA WA UMOJA WA MATAIFA WA MABADILIKO YA HALI YA HEWA NA TABIANCHI



## 3 FAHAMU ZAIDI: HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI, 2025



## KITAIFA

# MKUU WA MAKAPTENI ZANZIBAR AELEZEA MIPANGO YA SAFARI INAVYOTEGEMEA TAARIFA ZA HALI YA HEWA

**Zanzibar**




Mkuu wa Makapteni Zanzibar, Kapteni Kadadi Hassan Shea, alielezea namna taarifa za hali ya hewa zinavyowasaidia katika kupanga safari zao baharini na kuepukana na hasara zinazoweza kujitokeza.

Alizungumza hayo kupitia vyombo vya habari alipokuwa ametembelea banda la Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) katika maonesho ya Maadhimisho ya Siku ya Mabaharia Duniani yaliyofanyika katika viwanja vya Mnazi Mmoja, Zanzibar, Tarehe 22 hadi 25 Juni 2025.

“Taarifa za hali ya hewa zinatusaidia sana katika kufanya mipango ya safari zetu baharini ili kuepusha au kupunguza hasara zinazoweza kujitokeza, mfano kukiwa na utabiri wa uwepo wa upepo

mkali huwa tunajipanga kwa kuchukua mizigo kidogo katika kukabiliana nao, na kama kuna utabiri wa uwepo wa mvua tunachukua maamuzi ya kupakia mizigo, kama vile saruji, kwenye makontena," alielezea Kapteni Shea.




Kapteni Shea aliongezea kuwa maonesho haya yanawapa fursa mabaharia kukutana na kufahamiana na taasisi mbalimbali ili kuunganisha nguvu ya pamoja katika kuihudumia jamii kwa usalama na faida zaidi.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa TMA Ofisi ya Zanzibar, Masoud Makame Faki, alisema ushiriki wa Mamlaka katika maonesho hayo unajielezea kupitia kauli mbiu yake inayosema "Bahari Yetu, Wajibu Wetu na Fursa Yetu," ambapo kupitia kipengele cha "wajibu wetu" TMA inawajibika katika kuelezea namna huduma za hali ya hewa zinavyoweza kusaidia katika kuokoa maisha ya mabaharia, wasafiri na mali kwa ujumla.



## KIMATAIFA

# DKT. CHANG'A ASHIRIKI MKUTANO WA 62 WA KAMATI YA UTEKELEZAJI WA MKATABA WA UMOJA WA MATAIFA WA MABADILIKO YA HALI YA HEWA NA TABIANCHI

**Bonn, Ujerumani**



Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania katika Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi "Intergovernmental Panel on Climate Change (IPCC)", Dkt. Ladislaus Chang'a, alishiriki katika Mkutano wa 62 wa Kamati ya Ushauri na Kamati ya Utekelezaji chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi "United Nations Framework Convention for Climate Change (UN-FCCC)".

Mkutano wa 62 wa kamati hizo za UNFCCC ambazo ni: Kamati ya Ushauri katika masuala ya Sayansi na Teknolojia (Subsidiary Body for Scietific andTechnological Advice - SBSTA) na

Kamati ya Utekelezaji (Subsidiary Body for Implementation - SBI) ulifanyika Bonn, Ujerumani tarehe 16 hadi 26 Juni 2025, ambapo lengo lilikuwa ni kujadili mwenendo wa mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi, na hatua mbalimbali zinazohitajika kuchukuliwa na Nchi Wanachama katika kufikia malengo ya Mkataba wa UNFCCC, pamoja na Makubaliano ya Paris na itifaki ya Kyoto kuhusu Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi.

Mkutano huo ulifunguliwa tarehe 17 Juni, 2025 na Katibu Mtendaji wa UNFCCC, Simon Stiell ambapo katika hotuba yake ya ufunguzi, Bw. Stiel alisema majadiliano ya mkutano huo yana umuhimu wa kipekee katika kuokoa maisha ya mabilioni ya watu na shughuli za kiuchumi na kijamii duniani kote zinazoendelea kuathiriwa na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi. Alisema majadiliano ya kikao hicho yalitarajiwa kuleta suluhisho la uhakika la kutatua changamoto ya mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi dunia nzima kwa kuandaa mapendekezo stahiki yatakayowezesha kupunguza uzalishaji wa gesijoto na kuweka mikakati ya uhakika ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hew na tabianchi.

Viongozi wa Jopo la IPCC ni miongoni mwa wajumbe wa mkutano wa SBSTA na SBI ambapo jukumu la IPCC katika mkutano huo ni kutoa taarifa za kitafiti za sayansi ya mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi na mapendekezo yanayostahiki ya kuhimili na kukabiliana na mabadiliko hayo.

Mapendekezo ya Mkutano wa 62 wa Kamati za Ushauri za Mkataba wa UNFCCC (SBSTA na SBI)", yatawasilishwa, kujadiliwa na kutolewa mamuzi katika Mkutano Mkuu wa 30 wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi "United Nations Framework for Convention on Climate Change Conference of Parties (UNFCCC COP 30) ", unaotarajiwa kufanyika Novemba, 2025 nchini Brazil.

Dkt. Chang'a kwa nafasi yake ya Makamu Mwenyekiti wa IPCC alikuwa sehemu ya Ujumbe wa IPCC katika mkutano huo, ambapo Jopo la la IPCC liliwasilisha taarifa ya kisayansi kuhusiana na mwenendo wa mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi katika nchi mbalimbali duniani, ikiwemo Tanzania. Hivyo Dkt. Chang'a alitoa mchango wa taarifa za kitaalamu kuhusu Tanzania kupitia taarifa iliyowasilishwa kwa manufaa ya nchi yetu. Aidha, sambamba na mchango wake kupitia taarifa iliyowasilishwa na IPCC, Dkt. Chang'a alitekeleza vyema majukumu yake ya Makamu Mwenyekiti wa Jopo la IPCC na kuendelea kuiletea sifa nchi yetu.



JARIDA LA MWEZI

06 TOLEO NA. 056 JUNI 2025

TMA TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

## FAHAMU ZAIDI

### HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI, 2025

Kipindi cha mwezi Julai 2025, maeneo mengi ya nchi yanatarajiwa kuwa na hali ya baridi ya wastani hadi joto kiasi. Viwango vya chini zaidi vya joto vinatarajiwa kuendelea katika maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi. Kwa upande wa mvua, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache, hususan ukanda wa pwani, Ziwa Victoria na maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki na nyanda za juu kusini magharibi. Aidha, vipindi vya upepo mkali vinatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo, hususan ya ukanda wa pwani na maziwa makuu.

| MAENEO | MAELEZO |
|---|---|
| Pwani ya Kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 17 °C hadi 25 °C katika maeneo ya mwambao wa pwani na visiwani. Kwa maeneo ya nchi kavu kati ya nyuzi joto 13 °C na 21 °C. Kiujumla, hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi. **Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache ya mwambao wa pwani.** |
| Nyanda za juu Kaskazini Mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 10 °C hadi 18 °C katika maeneo mengi. Aidha, baadhi ya maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na viwango vya chini ya nyuzi joto 10 °C. **Kwa ujumla, hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi, huku vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa hususan katika maeneo ya miinuko.** |
| Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 14 °C hadi 21 °C katika maeneo mengi. Hata hivyo, maeneo ya miinuko ya mikoa ya Kagera na Geita yanatarajiwa kuwa na kiwango cha chini ya nyuzi joto 14 °C. **Aidha, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.** |
| Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 °C hadi 20 °C katika maeneo mengi. **Kwa upande mwingine, hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.** |
| Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 11 °C hadi 18 °C katika maeneo mengi. **Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.** |
| Nyanda za juu Kusini Magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 6 °C hadi 17 °C katika maeneo mengi. Aidha, hali ya baridi zaidi ya kiwango cha chini ya nyuzi joto 6 °C inatarajiwa katika maeneo ya miinuko, ikijumuisha mkoa wa Njombe. **Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi na vipindi vichache vya mvua hususan katika maeneo yenye miinuko.** |
| Pwani ya Kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 15 °C hadi 24 °C katika maeneo mengi. **Aidha, hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi pamoja na vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa kujitokeza katika maeneo machache ya mwambao wa pwani.** |
| Kanda ya Kusini (Mkoa wa Ruvuma): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 9 °C hadi 18 °C katika maeneo mengi. Maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na kiwango chini ya nyuzi joto 9 °C . **Hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi.** |

# MATUKIO KATIKA PICHA




*Waziri wa Maji, Mhe. Juma Aweso (MB), akipata elimu juu ya matumizi sahihi ya taarifa za hali ya hewa katika banda la Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani 2025.*



*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) iliungana na taasisi zingine zilizopo chini ya Wizara ya Uchukuzi kufanya usafi wa mazingira kwenye Uwanja wa Ndege wa Dodoma, ikiwa ni moja ya shughuli zilizoandaliwa na Wizara katika kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani 2025.*




*Waziri wa Nchi – Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene akipata elimu juu ya matumizi sahihi ya taarifa za hali ya hewa wakati wa maonesho ya kuadhimisha Wiki ya Utumishi wa Umma Dodoma, 2025.*



*Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kinyamwezi wakipata elimu juu ya namna Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) inavyofanya kazi zake katika ofisi kuu za utabiri, Dar es Salaam.*


JARIDA LA MWEZI
TOLEO NA. 055
MEI 2025
TMA
1 SULUHU MGAWANYO WA MAPATO WA HUDUMA ZA USAFIRI WA ANGA NCHINI YAPATIKANA
2 VIONGOZI NA WATAALAMU WA HALI YA HEWA WA ZIMBABWE WAFANYA ZIARA YA MAFUNZO YA SIKU TANO NCHINI TANZANIA
3 FAHAMU ZAIDI: HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI JUNI, 2025

**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA:**

**Mhariri**
Monica Mutoni

**Waandishi**
Wilbert Muruke
Godfrey Kazinja

**Msanifu Kurasa**
Kennedy Mgeta

**Shukrani**
Kituo Kikuu cha Utabiri
Ofisi ya Ushirikiano wa Hali ya Hewa Kimataifa

www.meteo.go.tz

@tmaservices

@tma_servces

@tanzaniameteorological

www.meteotz1950.blogspot.com

tanzaniametagency

TMAonline_TV

Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za
Kompyuta na Elimu Angavu,
1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27,
41218 DODOMA.